

# BARAZA LA HABARI TANZANIA



S.L.P 10160, Dar es Salaam, Tanzania  
Simu: +255 22 2775728/2771947  
Simu ya mkononi: +255 719 494640  
+255 767 494826/  
Barua pepe: media@mct.or.tz  
Tovuti: <http://www.mct.or.tz>  
S.L.P 3490, Zanzibar

P.O.Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania  
Tel: +255 22 2775728/2771947  
Mob: +255 719 494640  
+255 767 494826/  
Email: media@mct.or.tz  
Website: <http://www.mct.or.tz>  
P.O.Box 3490, Zanzibar

## TAARIFA KUHUSU KUIBUKA KWA MWENDELEZO WA MATUKIO YA UNYANYASAJI WA WAANDISHI WA HABARI WAKIWA WANATIMIZA MAJUKUMU YAO

Baraza la Habari Tanzania (MCT), limefedheheshwa sana na linalaani kuendelea kwa matukio ya unyanyasaji wa waandishi wa habari unaofanywa na vyombo vya dola, baadhi ya viongozi wa serikali pamoja na wananchi.

Licha ya maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu vyombo vya habari vilivyofungiwa nchini Tanzania kufunguliwa na kuendelea na majukumu yake, bado hali ya uminywaji wa uhuru wa habari na wanahabari imeendelea katika kipindi cha siku 15 toka hotuba yake ya kuwaapisha makatibu wakuu, manaibu makatibu wakuu na wakurugenzi wa taasisi.

Jumanne ya Aprili 6, 2021, Rais Samia, aliagiza Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuvifungulia vyombo vya habari vilivyofungiwa na kuagiza wahusika kutotumia ubabe kuvidhibiti.

“Nasikia kuna vyombo vya habari mlivifungia, vifungulieni na vifuate sheria tusiwape mdomo kwamba tunaminywa uhuru wa kuzungumza. Tusifungie kibabe wafungulieni na kuhakikisha wanafuata kanuni na miongozo ya serikali,” Rais Samia aliagiza.

Tafsiri iliyo wazi ya maagizo ya Rais ni kwamba hapendezwi na hali hii ya unyanyasaji wa vyombo vya habari na wanataaluma wake. Baraza linashangazwa na hali inavyokwenda hivi sasa maana mara baada ya maagizo ya Rais, vitendo vya ukiukwaji wa haki za waandishi vimeshamiri kinyume na matarajio ya Watanzania. Tunajiuliza ni nani kati ya wananchi na watendaji ambaye hakumwelewa Rais.

Matukio ya uvunjifu wa haki za wanahabari ni pamoja na lile la Aprili 12, 2021 ambalo lilitokea jijini Dar es Salaam ambapo waandishi wa habari Christopher James wa ITV & Radio One na Dickson Billikwija wa Island TV waliwekwa chini ya ulinzi wa polisi kwa maagizo ya Mkurugenzi wa Temeke Bw. Lusabilo Mwakabibi, kwa tuhuma za kuvamia mkutano wa kiongozi huyo.

Tukio jingine lilitokea huko Mwanza Aprili 09, 2021 ambapo Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana Dk. Philis Nyimbi, alimtishia mwandishi wa habari kuwa atamfanyia kitu ambacho kitasababisha aachishwe kazi, kutokana na mwandishi huyo, Bw. Mabere Makubi wa ITV kuandika habari ambazo mkuu huyo wa wilaya alisema zinahatarisha ajira yake.

Aprili 12, 2021 mwandishi wa habari wa kujitegemea anayeandikia gazeti la The Guardian kutokea mjini Moshi, Bw. James Lanka alikamatwa na polisi na kuwekwa mahabusu kwa siku tatu mfululizo bila kufunguliwa mashtaka wala kuchukuliwa maelezo, baada ya kuhoji sababu za wafanyabiashara kukamatwa bila utaratibu kufuatwa.

Tukio jingine lilitokea mkoani Katavi ambapo mwandishi wa habari wa kituo cha runinga cha Channel 10, Bw. Pascal Katona ambaye alihudhuria shughuli za uchaguzi wa Imamu wa Msikiti wa Makanyagio ulioko Manispaa ya Mpanda kwa ajili ya kupata taarifa na kuuhabarisha umma juu ya matokeo ya uchaguzi huo, alivamiwa na wananchi ambao hawakukubaliana na matokeo ya uchaguzi huo, na kumshambulia na kumharibia vitendea kazi vyake.

Bado tena kuna tukio la Aprili 21, 2021 huko Zanzibar, pale mwandishi wa habari wa gazeti la Mwananchi, Jesse Mikofu aliposhambuliwa na askari wa JKU wakati akifanya kazi yake ya uandishi wa habari.


Mwandishi huyo alikutana na zahama hiyo baada ya kuwapiga picha askari waliokuwa wakiwakamata na kuwaondoa wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu kama *dada njoo* ambao wanatakiwa kuondoka eneo la Darajani na kwenda Kibandamaiti.

Mwandishi huyo alipopiga picha alikamatwa na kisha simu yake ambayo ndiyo alikuwa akiitumia kufanyia kazi kuharibiwa na mwandishi mwenyewe kuteswa na kujeruhiwa.

Baraza la Habari linalaani vitendo hivi vya ukatili kwa waandishi wa habari ambavyo hata Mhe. Rais Samia S. Hassan ameonyesha kutopendezwa navyo na kuonya dhidi ya matumizi ya ubabe.

Baraza linapenda kuvikumbusha vyombo vya ulinzi na usalama, viongozi wa serikali na wananchi kwa ujumla, kuwa uandishi wa habari sio tu ni kazi halali, bali pia ya muhimu sana kwa jamii yetu. Sote hatuna budi kuiheshimu tasnia hii na kuipa ushirikiano wakati wote utakapohitajika.

Pia Baraza linawakumbusha kuwa maagizo ya Mhe. Rais Samia kuhusu uhuru wa vyombo vya habari na kuheshimu sheria havina budi kufuatwa na kutekelezwa kwa vitendo. Kuendelea kuwaumiza waandishi wa habari na kuminya uhuru wa vyombo vya habari, ni kwenda kinyume na agizo la Rais na hauleti picha nzuri kwa Taifa letu ndani na nje ya nchi.



Kajubi D. Mukajanga  
Katibu Mtendaji

Imetolewa leo tarehe 22.04.2021